BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Kwanza – Tarehe 12 Februari, 2025.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 6 Disemba, 2024.

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji Leseni za Biashara, Nam. 13 ya 2013 na Kutunga Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Utoaji Leseni za Biashara Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji Leseni za Biashara, Nam. 13 ya 2013 na Kutunga Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Utoaji Leseni za Biashara Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

22\. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali inachukua hatua gani stahiki za kuona kwamba wanafunzi na watoto walio chini ya umri wa miaka 18 hawashiriki kwenye kumbi za starehe kama vile Chukwani na Mjini Joto.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

10\. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kuwa mwenendo wa mikopo ya kausha damu mara nyingi inarejesha nyuma maendeleo ya wajasiriamali hasa kinamama.

(a) Je, Wizara yako ina mkakati gani katika kuwanusuru wananchi ili kuondokana na changamoto zinazotokana na mikopo hiyo.

(b) Ni utaratibu upi wa kisheria unaohalalisha kuwepo na kuongezeka kwa mikopo hiyo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

63\. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunaipongeza sana Serikali kwa ujenzi wa kiwanda cha mwani kilichopo Chamanangwe kisiwani Pemba, kiwanda ambacho kinalenga kuboresha hali za wajasiriamali wetu hususani wazalishaji wa mwani nchini.

(a) Je, kwa sasa maendeleo ya kiwanda hicho yako vipi.

(b) Ni lini hasa Serikali imepanga kiwanda hiki kuanza uzalishaji wake.

**<u>Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

6. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

   Ni yepi matarajio ya uwekezaji katika tasnia ya filamu kwa muigizaji nguli wa filamu duniani anaejulikana kwa jina la Idriss Elba.

38. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

   Naipongeza Serikali kwa uamuzi wake mzuri wa kujenga nyumba ya kisasa ya sanaa iliyopo katika eneo la Mkwe Zanzibar.

   Je, ni yepi malengo na matarajio ya ujenzi wa nyumba hiyo.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

3. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

   Ni yepi matarajio ya Wizara katika kuhakikisha kwamba watalii wanaokuja nchini wanapata huduma za afya zenye ubora wa viwango vya kimataifa ili kuwa na uhakika wa kuweza kurejea tena nchini.

4. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.

   Kumejitokeza malalamiko kwa baadhi ya watalii wanaoitembelea nchi yetu kukuta vivutio vilevile kila wanapokuja nchini.

   Je, Wizara imejipanga vipi katika kufanya ubunifu wa kuviboresha na kuviongeza vivutio vyetu vya utalii ili viende na wakati zaidi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

25. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Zao la mbaazi ni miongoni mwa mazao yenye uhitaji mkubwa katika soko la nje.

    Kwa kiasi gani Wizara yako inawasaidia na kuwahamasisha wakulima wa zao hili, ili kunufaika na fursa hiyo.

132. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

     Mpango mkuu wa sekta ya kilimo ni upi kwa sasa.

**Wizara ya Afya:**

66. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Ni asilimia ngapi ya watoto wanaopata changamoto za udumavu na ni zipi athari za udumavu katika maendeleo ya baadae kwa mtoto aliyeathirika.

84. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Kumekuwa na wimbi kubwa la wagonjwa kutoka ngazi za shehia na wadi wanaokimbilia kupata huduma za afya katika hospitali za Wilaya na hospitali za Rufaa, kutokana na kuwepo kwa huduma duni za afya kwenye zahanati zilizopo ngazi za chini karibu nchi nzima.

    Je, ni upi Mpango na Mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa Wizara yako wa kuondosha tatizo hilo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

46. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni kwa namna gani Serikali inaendelea na mikakati itakayosaidia kupatikana wanasayansi wenye uweledi na tija kwa maslahi ya taifa letu.

150. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kigezo cha uzoefu na wingi wa ufaulu wa wahitimu katika vyuo vyetu imekuwa kikwazo kikubwa cha wao kufanikiwa kupata ajira.

(a) Je, Serikali inaichukulia kwa jicho gani changamoto hii.

(b) Je, Wizara haioni kwamba ile sera ya elimu ya *"education for self-reliance"* kwa sasa huenda ikawa ni suluhisho bora la kupambana na ajira kwa wahitimu wetu katika vyuo mbali mbali.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

20. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Huduma za simu kupitia makampuni yao huwa na namba za dharura kwa wateja wao ambazo zinasaidia kutatua changamoto za wateja.

Je, Wizara yako inao utaratibu wa kuwapatia watalii wetu namba maalumu itakayowasaidia pindi wakipata changamoto yoyote.

92. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Licha ya elimu na miongozo mbali mbali inayotolewa na Serikali bado suala la uvamizi wa maeneo ya hifadhi za barabara limekuwa changamoto kubwa hapa Zanzibar.

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya changamoto hii hususan kwa maeneo ya miji mipya mbali mbali inayoibuka hivi sasa.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

48. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ni wazi kuwa rasilimali za Uchumi wa Buluu ni pamoja na bahari, maziwa, mito, mabwawa, maji chini ya ardhi, madini, samaki, gesi na mafuta.

Ni kwa kiasi gani uwepo wa rasilimali hizi za uchumi wa buluu, utachangia kupatikana fursa za kutosha za ajira hapa nchini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji Leseni za Biashara, Nam. 13 ya 2013 na Kutunga Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Utoaji Leseni za Biashara Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**12 Februari, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**